

# Vidokezo vyat Kuwasilisha Maombi kwa Shule ya Gavana (*Governor's School*)

---

## Maombi na Insha

- Inapaswa kupigwa chapa kwa kutumia Times New Roman, kuwekwa kitambulisho kulingana na miongozo ya maombi na kuchapishwa.
- Insha ni sehemu muhimu katika mchakato wa uteuzi. Pata mtu mzimaakupe maoni kuhusu insha zako ili uweze kuwasilisha muundo ulioandikwa vizuri.
- Mambo ya kufikiria:
  - Je, maudhui yanashughulikia maelekezo ya insha?
  - Je, inalenga maelekezo na imepangwa kwa njia ya kimantiki?
  - Je, kuna mifano na ufanuzi wa kusaidia majibu?
  - Je, imeandikwa vizuri BILA makosa yoyote ya kisarufi na ya tahajia

## Fomu ya Utayari wa Kibinafsi

- Orodhesha ushiriki, tuzo, heshima katika maeneo yafuatayo:
  - Kitaaluma (orodha rasmi ya heshima, Jamii za Heshima, Kata zote, AIMS *Biomedical*, nk)
  - Kuhusiana na huduma (Klabu ya Beta, Baraza la Wanafunzi, Tuzo za Raia, huduma -shughuli za kujifunza, NCNAYO, JROTC, Kamati ya Pow Wow, nk)
  - Riadha (nafasi za nahodha, chaguzi za Kata zote, AAU, densi, shabiki, Mkanda Mweusi katika Judo, Densi ya Timu, Timu ya Densi ya Jamii, nk.)
  - Ushiriki wa Jamii (Skauti za Wavulana, Skauti za wasichana, shughuli za kanisa, Jack & Jill, GLAAD, Kilabu cha Wavulana na Wasichana, nk)
  - Ajira (sehemu ya muda, idadi ya masaa)
  - Majukumu ya nyumbani (kutunza ndugu zako wadogo)
- Jumuisha nafasi zozote za uongozi ambazo uliwahi shikilia (mwenyekiti wa kamati, afisa, nahodha wa timu). Je, ushiriki wako katika shughuli hizi umekuandaa vipi kwa uzoefu wa Shule ya Gavana?

## Mapendelekezo

- HAKUNA MZAZI, JAMAA, au MWANAFUNZI anayefaa kuwasilisha pendekezo.
- Lazima uwe na fomu MBILI za pendekezo zilizokamilishwa na watu ambaow wanaweza kuzungumzia kuhusu uwezo wako katika eneo la uteuzi.
- Angalau pendekezo MOJA lazima itoke kwa mwalimu wa shule ya upili, ikiwezekana katika eneo la uteuzi. Sio lazima awe mwalimu wako wa sasa; lakini inapaswa itoke kwa mwalimu wa shule ya upili ambaye anaweza kuzungumzia kuhusu udadisi wako wa akili, upendo wa kujifunza, na uwezo wa kufaidika kutokana na uzoefu wa Shule ya Gavana.
- Uliza mapema vyat kutosha ili wapendekezaji wapate muda wa kukamilisha fomu.
- Uliza ikiwa mtu huyo anajisikia huru kujaza pendekezo chanya kukuhusu.